**KAULI YA FARAGHA YA WORLDCOIN**

Asante kwa kuchagua kuwa mmoja wa Jamii ya Worldcoin!

Kauli hii ya Faragha inasimamia data unazotupatia kupitia matumizi yako ya tovuti, programu, na mfumo wa Worldcoin, na pia huduma nyingine zinazohusiana na Kauli hii ya Faragha (kwa pamoja, "Huduma"). Sehemu ya 4 hapa chini inabainisha data tunazokusanya na kwa nini. Kauli hii ya Faragha imejumuishwa kwenye na inatawaliwa na Sheria na Masharti ya Mtumiaji wa Worldcoin (getworldcoin.com/terms).

Ili kupata maelezo kuhusu jinsi tunavyokusanya, kutumia, kuhifadhi, na kufuta data zako za bayometriki zilizokusanywa kupitia Orb yetu, tafadhali pitia Fomu ya Idhini ya Data, iliyojumuishwa kama rejeleo. Hatutakusanya data zako za bayometriki isipokuwa iwe umekubaliana na Fomu ya Idhini ya Data.

**1. Visasisho vya Kauli hii ya Faragha**

Wakati mwingine tunasasisha Kauli hii ya Faragha. Tukifanya mabadiliko makubwa, kama vile jinsi tunavyotumia maelezo yako ya kibinafsi, basi tutakuarifu kupitia barua pepe au ujumbe katika app yako ya Worldcoin.

**2. Nini kiko ndani ya Kauli hii ya Faragha?**

- Jitihadi zetu za kulinda faragha yako na data zako
- Maelezo tunayokusanya na kwa nini
- Jinsi tunavyotumia data tunazokusanya
- Mahali ambako tunasindika data zako
- Wakati ambao tunashiriki data zako
- Jinsi data zako zinavyorekodiwa kwenye blockchain ya umma
- Jinsi tunavyotumia kuki
- Muda tunaohifadhi data zako
- Jinsi Kauli hii ya Faragha ilivyo tofauti kwa watoto na vijana
- Jinsi ya kuwasiliana nasi kuhusu Kauli hii ya Faragha

**3. Jitihadi Zetu za Kulinda Faragha yako na Data zako**

Tunajitahidi kwa dhati kulinda faragha yako na kulinda data zako:

**Usiri**

Tumebuni bidhaa na huduma haswa tukijali faragha yako. Tunapokusanya

data, tunafanya hivyo ili kuboresha bidhaa na huduma zetu. Kila wakati tunakueleza, hapa katika Kauli hii ya Faragha au katika fomu za idhini ya data za bidhaa na huduma maalum, ni data gani tunakusanya, kwa nini tunakusanya data hizo, na tunachofanya na data hizo.

**Usalama wa Data**

Tumeteua timu ya kutunza data zako na tumeweka kinga halisia na za kielektroniki zinazolinda data zako zinaposafirishwa na zinapohifadhiwa. Wakati huo huo, hakuna huduma inayoweza kuwa salama kabisa - ikiwa una wasiwasi zozote kuhusu akaunti yako au data zako, tafadhali wasiliana nasi kupitia Lango letu la Maombi au kwa kututumia barua kwa anwani Tools For Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA.

Jitihada zetu kwa faragha yako na usalama za data zako ni zaidi ya inavyohitajika na sheria na zaidi ya kauli nyingi za faragha. Katika

Worldcoin, tunatambua kwamba tunaweza tu kutimiza misheni yetu ya kusambaza Worldcoin kwa njia ya haki kwa watu wengi kadri iwezekanavyo ikiwa watu watakuwa na imani nasi, na faragha na usalama wa data ni jambo la msingi ili kupata imani yako.

**4. Maelezo Tunayokusanya na Kwa Nini**

**4.1 Data Unazotupatia**

Wewe kama mtumiaji, hauhitajiki kupatia data zozote ili kufikia app ya Worldcoin. Hata hivyo, unaweza kuhitajika kutupatia data fulani ili uweze kutumia kipengele fulani ndani ya Huduma. Hapa chini kuna orodha ya data unazoweza kupatiana na tunachoweza kufanya na data hizo:

- **Jina la kwanza na la mwisho:** Unaweza kuchagua kuweka jina lako ili kulihusisha na akaunti yako. Worldcoin pamoja na watumiaji wengine huenda wakaona jina lako unapoamua kutangamana na akaunti yako. Huenda tukahitaji jina lako unapowasilisha ombi la data za mhusika.
- **Anwani ya barua pepe:** Unaweza kuchagua kuweka anwani yako ya barua pepe ili kuihusisha na akaunti yako. Huenda tukahitaji anwani yao ya barua pepe unapowasilisha ombi la data za mhusika.
- **Nambari ya simu:** Unaweza kuchagua kuweka nambari yako ya simu ili kuihusisha na akaunti yako. Kwa kibali chako, watumiaji wengine wanaweza kutafuta akaunti yako kwa kutumia nambari yako ya simu. Huenda tukahitaji nambari yako ya simu unapowasilisha ombi la data za mhusika.
- **Maoni na mawasiliano kutoka kwako:** Hii inajumuisha barua pepe zozote, ujumbe wowote, au mawasiliano mengine yoyote unayotutumia kupitia barua pepe au tovuti za mitandao ya kijamii ya wahusika wengine.
- **Waasiliani katika kitabu cha anwani:** Unaweza kuturuhusu kufikia kitabu chako cha anwani ili kuwezesha kipengele ambacho kinakurahisishia kutafuta na kutangamana na watumiaji wengine ambao huenda wakawa katika kitabu chako cha anwani.

**Tafadhali kumbuka:** Una jukumu la kuhakikisha kwamba kushiriki maelezo yako ya mawasiliano yanaambatana na sheria husika. Hii inaweza kukuhitaji kupata kibali cha waasiliani wako. Pia tunaweza kupata maelezo kukuhusu wewe kutoka kwa watumiaji wengine wanaoleta au kuweza waasiliani wao. Tunatumia na huenda tukahifadhi maelezo haya ya mawasiliano ili kukusaidia wewe na waasiliani wako kutangamana kupitia Huduma zetu. Unaweza kubadili uamuzi wako na kuondoa uwezo wetu wa kufikia waasiliani wako wakati wowote katika mipangilio ya kifaa chako. Ukichagua kuleta waasiliani katika kitabu cha anwani cha kifaa chako ili kujua ni waasiliani wagani wanatumia Huduma zetu au ili kuwaalika wajiunge nawe katika kutumia Huduma zetu, mara kwa mara tutalandanisha maelezo ya waasiliani wako, pamoja na nambari ya simu na barua pepe, kwenye seva zetu.

Ikiwa una uhusiano wa kibiashara nasi (kama vile wewe ni Mhudumu wa Orb au mletaji wetu), basi tunaweza kuhitaji maelezo kama vile majina, anwani ya barua, barua pepe, nambari ya simu, anwani ya pochi, na nyaraka zingine (kama vile kitambulisho chako cha serikali) kama sehemu ya kuimarisha uhusiano huo wa kibiashara na ili kutimiza majukumu ya kumjua-mteja-wako. Tunaweza kutumia huduma za wahusika wengine, kama vile Onfido, ili kutusaidia kukusanya na kuhakiki maelezo na nyaraka zilizotajwa hapa juu ili kutimiza majukumu ya kumjua-mteja-wako.

**4.2 Data Tunazokusanya Kutoka Kwa Vyanzo Vingine**

Mara kwa mara, huenda tukapata maelezo kukuhusu wewe kutoka kwa vyanzo vingine vifuatavyo:

- Data za Blockchain. Tunaweza kuchambua data za blockchain ya umma ili kuhakikisha kwamba watu wanaotumia Huduma zetu hawajihusishi katika shughuli haramu au zilizopigwa marufuku chini ya Makubaliano yetu ya Mtumiaji wa Worldcoin, na ili kuchambua mitindo ya miamala kwa madhumuni ya utafiti na utengenezaji.
- Huduma za Uthibitishaji Utambulisho. Tunaweza kupata maelezo kutoka kwa huduma za wahusika wengine kwa kutumia data zako ili kuthibitisha utambulisho wako ikiwa inahitajika na sheria (kama vile mahitaji husika ya kumjua-mteja-wako). Ili kufafanua, **hatutumii** data zako za bayometriki tunapothibitisha utambulisho wako kama inavyohitajika na sheria.

**4.3 Maelezo ya Eneo**

Ykiamua kuwezesha huduma inayotegemea eneo (kama vile kipengele kinachokuruhusu kumpata Mhudumu wa Orb aliyekaribu nawe),

basi tunaweza kukusanya maelezo kuhusu eneo lako ili tuweze kukupa huduma hiyo. Eneo lako linaweza kubainishwa kwa kutumia:

- GPS
- Anwani ya IP
- Maelezo kuhusu minara iliyo karibu nawe ya mitambo ya simu na maelezo ya kituo cha ya Wi-Fi kilicho karibu nawe

Aina ya maelezo ya eneo yanayokusanywa inalingana na huduma unayotumia, kifaa unachotumia (kwa mfano, Apple au Android), na mipangilio ya kifaa chako (iwe vibali vimewezeshwa au kulemazwa). Unaweza kubadilisha vibali vyako wakati wowote katika mipangilio ya kifaa chako.

**4.4 Data Tunazokusanya Kiotomatiki**

Tukiruhusiwa chini ya sheria husika, tunaweza kukusanya aina fulani za data kiotomatiki unapotumia Huduma zetu. Maelezo haya yanatusaidia kuangazia masuala ya uhudumiaji wateja, kuimarisha utendakazi wa Huduma, kukupa huduma fanisi na ya kibinafsi, na ili kulinda maelezo ya kuingia kwenye Akaunti yako. Maelezo yanayokusanya kiotomatiki yanajumuisha:

- **Vitambulishaji vya Mtandaoni**: Maelezo ya eneo la kijiografia (tazama hapa juu), mfumo msingi wa uendeshaji kompyuta au simu tamba, jina na toleo la kivinjari, na anwani za IP
- **Data za Matumizi**: Data za uthibitishaji, maswali ya kiusalama, machapisho ya mitando ya kijamii ya umma, na data nyingine zilizokusanywa kupitia kuki na teknolojia sawia

Hivyo hivyo, programu tamba ya Worldcoin inakusanya maelezo kwa ajili ya usuluhishaji matatizo na uimarishaji. Tunatumia huduma za wahusika wengine, kama vile Segment.io au PostHog, ili kufanya makadirio ya maelezo kuhusu matumizi ya watumiaji. Inapowezekana, tunachukua hatua ili kupunguza au kuficha maelezo yanayotumwa kwa wahusika wengine (kama vile kusimba data).

**4.5 Data Bila Utambulisho na Zilizokadiriwa**

Uondoaji utambulisho ni mbinu ya kusindika data ambayo hubadilisha data za kibinafsi ili zisiweze kuhusishwa na mtu fulani. Mifano ya data bila utambulisho zinajumuisha:

- Data za miamala
- Data za ubonyezaji maeneo ya skrini
- Metriki za utendakazi
- Viashiria ulaghai

Pia tunakadiria data, kwa kuunganisha pamoja viwango vikubwa vya maelezo ili yasimtambulishe tena wala kumrejelea mtu binafsi. Tunaweza kutumia data bila utambulisho au zilizokadiriwa kwa madhumuni yetu ya kibiashara, kama vile kuelewa mahitaji na tabia za watumiaji, kuimarisha Huduma zetu, kufanya shughuli za umaizi na uuzaji wa kibiashara. kugundua hatari za kiusalama, na kufunza teknolojia zetu.

**4.6 Data za Bayometriki**

Tutakusanya tu na kutumia data zako za bayometriki baada ya wewe kukubaliana na Fomu ya Idhini ya Data, ambayo inaelezea kwa kina aina za data za bayometriki tunazosindika na kwa nini. Data za bayometriki **hazihusishwi** na data za akaunti yako katika Sehemu ya 4 hapa juu.

**5. Jinsi Tunavyotumia Data Tunazokusanya**

Ni lazima tuwe na sababu halali (au “msingi wa kisheria wa kusindika”) ya kutumia maelezo yako za kibinafsi. Inapohusu data zako za bayometriki, tunakuomba idhini yako moja kwa moja. Hata hivyo, wakati unatutarajia sisi kutumia maelezo yako ya kibinafsi na matumizi yetu ya maelezo hayo yanaambatana na sheria husika, hatukuombi kibali chako.

Tunatumia tu maelezo yako kwa malengo ya aina zifuatazo:

- Kukupa Huduma zetu, na pia maelezo kuhusu Huduma zetu;
- Kufanya utafiti ili kuimarisha na kuboresha bidhaa zetu;
- Kufunza teknolojia yetu ili iweze kutambua watumiaji binafsi vyema zaidi;
- Kuchambua matumizi yako ya Huduma zetu ili kukupa usaidizi bora;
- Kutumia anwani ya pochi lako ili kukutumia sarafu za WLD au sarafu nyingine za kidijitali ambazo tunahusika nazo;
- Kuambatana na sheria husika (kama vile kutumia anwani yako ya IP ili kuwazuia watu binafsi kutoka mataifa au nchi zilizopigwa marufuku kutumia Huduma);
- Kushughulikia maombi, malalamishi na maswali yako;
- Kusuluhisha migogoro, kutatua masuala, na kutekeleza makubaliano yetu nawe, pamoja na Kauli hii ya Faragha na Makubaliano ya Mtumiaji wa Worldcoin; na
- Kuwasiliana nawe kuhusiana na visasisho kwenye Huduma.

**6. Mahali Ambako Tunasindika Data Zako**

**Tafadhali kumbuka:** Unapotupatia data zako, huenda zikatumwa, kuhifadhiwa, au kusindikwa katika eneo nje ya mahali ambako data zako zilikusanywa. Nchi ambako data zako zinatumwa, kuhifadhiwa, au kusindikwa huenda zikawa hazina sheria za ulindaji data ambazo ni sawa na zile za nchi ambako ulikuwa wakati ulipatiana data.

Tunaambatana na misimamo iliyotajwa katika Kanuni Jumla ya Ulinzi wa Data (General Data Protection Regulation, GDPR), hata wakati hatuhitajiki. Kwa mfano, wakati tunashirikiana na wasindikaji data wanaoendesha biashara yao nje ya Eneo la kiuchumi la Ulaya (European Economic Area, EEA) na Uingereza, tunahakikisha kwamba wanaambatana na GDPR na Sheria ya Ulindaji Data ya Uingereza (UK Data Protection Act) ya 2018. Tunashiriki tu data na wasindikaji data walio nje ya EEA na Uingereza, ikiwa utumaji huo wa data ni wa kisheria na ikiwa tuna imani kwamba msindikaji data huyo atalinda data zako kama inavyohitajika chini ya sheria husika na, aidha, kwa kuambatana na viwango vya Worldcoin.

**7. Wakati ambao Tunashiriki Data Zako**

**Hatutawahi kuuza data zako**.

Wakati ambapo tunashiriki data zako nje ya Worldcoin, kila wakati:

- Tunazishiriki kwa njia salama;
- Tunahakikisha kwamba inashughulikiwa kwa njia ambayo inaendanisha na jitihada zetu kwa faragha yako; na
- Tunazuia kampuni zingine kutozitumia kwa malengo yako ya uuzaji.

Tunashiriki data zako, na watu walio ndani ya Worldcoin na wale walio nje ya Worldcoin, kwa njia hizi chache:

- **Kushiriki Ndani ya Worldcoin:** Tunafichua tu data kwa wanatimu wa Worldcoin ambao wanahitaji kuzifikia ili kuweza kufanya kazi na majukumu yao. Tunafichua tu kiwango cha data ambacho kinahitajika ili kufanya kazi na majukumu fulani.
- **Kushiriki na wachuuzi na watoa huduma nje ya Worldcoin:** Tunafichua tu data kwa watoa huduma ambao huduma zao tunazitegemea ili kusindika data na kukupa Huduma zetu. Tunafichua tu data kwa Wachuuzi wa Huduma ya Uthibitishaji Utambulisho ikiwa inahitajika na Sheria (yaani, mahitaji-ya-kumjua-mteja-wako). Data tunazowapatia Wachuuzi wa Huduma ya Uthibitishaji Utambulisho hazijumuishi data za bayometriki.
- **Kushiriki na maafisa wa utekelezaji sheria, maafisa, au wahusika wengine:** Tunaweza kufichua data zako ili kuambatana na sheria husika na kutii mahitaji ya lazima ya kisheria. Kwa uangalifu tunazingatia kila ombi ilikubaini kana kwamba ombi hilo linaambatana na sheria, na hatutasitasita kupinga maombi ambayo si halali, yanayopita mpaka, au yasiyo ya kisheria. Tutashiriki tu data zako na watekelezaji sheria, maafisa na wahusika wengine ikiwa tunalazimishwa na amri ya hakimu, amri ya

mahakama, au utaratibu sawa.

- Tunaweza kufichua data zako wakati tunapoamini kwa nia nzuri kwamba ufichuaji huo ni muhimu ili kuzuia madhara kwetu au kwa wengine, ili kuripoti shughuli inayotuhumiwa kuwa haramu, ili kuchunguza ukiukaji wa Makubaliano ya Mtumiaji wa Worldcoin na sera nyingine husika, au ili kutekeleza makubaliano kama hayo na ili kutekeleza makubaliano kama hayo.

**8. Jinsi Data Zako Zinavyorekodiwa kwenye Blockchain ya Umma**

Maelezo ya miamala yanayohusiana na matumizi yako ya huduma za Worldcoin yanaweza kurekodiwa katika blockchain ya umma.

**Tafadhali kumbuka:** Blockchain nyingi ziko wazi kufanyiwa uchambuzi wa kiuchunguzi, ambao unaweza kupelekea utambulisho kujulikana na ufichuaji wa maelezo ya kifedha ya kibinafsi. Data za blockchain (kama vile anwani ya pochi au anwani ya IP) zinaweza kuunganishwa na maelezo ya kibinafsi, na kuifanya iwezekane kuhusisha miamala katika blockchain ya umma na mtu maalum.

**9. Jinsi Tunavyotumia Kuki**

Tunatumia kuki ili kusaidia Huduma zetu kufanya kazi vyema zaidi. Kando na kuki, tunaweza kutumia teknolojia nyingine sawa na hiyo, kama vile web beacons, ili kuwafuatilia watumiaji wa Huduma zetu. Web beacons, (pia zinaitwa "clear gifs") ni grafiki ndogo sana zilizo na kitambulishi cha kipekee, zilizo na utendaji sawa na kuki. Zinatumiwa kufuatilia mwenendo wa watumiaji tovuti mtandaoni.

Tofauti na kuki, ambazo zinahifadhiwa kwenye hifadhi au kifaa cha mtumiaji, clear gifs zimewekwa kwenye kurasa za tovuti kwa njia ambazo hazionekani na zina ukubwa wa kikomo kilicho mwishoni mwa sentensi hii. Sisi na watoa huduma wetu wengine tunatumia beacons kwa sababu zilizotajwa hapa chini, lakini cha msingi ni ili kusaidia kudhibiti vyema zaidi maudhui yaliyo kwenye Huduma zetu kwa kutufahamisha ni maudhui gani fanisi.

Pia tunaweza kutumia kuki zinazoitwa "Flash Cookies" (pia zinajulikana kama "Local Shared Objects” au "LSOs") ili kukusanya na kuhifadhi maelezo kuhusu matumizi yako ya huduma zetu, kuzuia ulaghai na kuwezesha utendakazi mwingine wa tovuti.

Kwa pamoja, zana hizi zinatuwezesha:

• Kufanya uchambuzi wa tovuti;

• Kuzuia ulaghai na kuzuia mashambulizi dhidi ya tovuti na Huduma zetu; na

• Kutangaza Huduma zetu, na bidhaa na huduma za ziada kutoka kwa wabia wetu wengine.

Tunatumia kuki na vifuatiliaji ili kukupa kitambulisho cha kipekee ili tuweze kurekodi:

• Tovuti unazotembelea

• Muda uliotumia kuvinjari, pamoja na kiwango cha muda ambacho tangazo au ukurasa wa tovuti uliweza kuonekana

• Anwani yako ya IP

Unaweza kuzuia kuki wakati wowote kwa kutumia mipangilio ya kivinjari chako, lakini kufanya hivyo huenda kukawekea vikwazo huduma yako ya kuvinjari na uwezo wako wa kutumia vipengele fulani vya Huduma. Kwa sasa haturuhusu ishara za kivinjari za “Do Not Track” au DNT au mbinu yoyote nyingine ambayo inawasilisha kiotomatiki chaguo lako la kutofuatilia mtandaoni.

Tunatumia aina zifuatazo za kuki:

**Kuki Muhimu Sana:** Kuki hizi ni muhimu ili Huduma zifanye kazi na haziwezi kuzimwa katika mifumo yako. Kwa kawaida huwa zimepangwa kukabiliana na hatua unazofanya ambazo zinajumuisha kuomba huduma, kama vile kupanga mapendeleo yako ya faragha, kuingia kwenye akaunti yako, au kujaza fomu. Hizi pia zinajumuisha kuki ambazo tunaweza kutegemea katika kuzuia ulaghai. Unaweza kupanga kivinjari chako kuzuia au kukuarifu kuhusu kuki hizi, lakini huenda baadhi ya Huduma zikakosa tufanya kazi.

**Kuki za Utendakazi/Uchambuzi:** Kuki hizi zinatuwezesha kuhesabu mara ya kutembelea na vyanzo vya trafiki ili tuweze kupima na kuimarisha utendakazi wa Huduma zetu. Zinatusaidia kujua umaarufu wa ukurasa na jinsi wageni wanavyovinjari Huduma. Maelezo yote yanayokusanywa na kuki hizi yamekadiriwa na kwa hivyo hayana utambulisho. Ukikosa kuruhusu kuki hizi, hatutajua wakati umetumia Huduma zetu, na hatutaweza kufuatilia utendakazi wake.

**Kuki za Utendakazi:** Kuki hizi zinatuwezesha kukumbuka machaguo uliyofanya na kubinafsisha Huduma zetu ili tuweze kukupa maudhui muhimu kwako. Kwa mfano, kuki ya utendaji inaweza kukumbuka mapendeleo yako (k.m. chaguo la nchi au lugha), au jina lako la mtumiaji.

**Kuki za Matangazo:** Worldcoin inatumia watoa huduma wengine ili kuonyeshana matangazo kwenye Huduma zetu na kuweka matangazo kwenye tovuti za wahusika wengine ambayo yanaweza kuwa muhimu kwako au kukuvutia. Kuki hizi pia zinatumika kusaidia kupima ufanisi wa kampeni za matangazo. Zinakumbuka kwamba umetembelea tovuti na maelezo haya yanaweza kushirikiwa na mashirika mengine, kama vile watangazaji. Hii inamaanisha kwamba baada ya kuwa kwenye tovuti zetu, unaweza kuona matangazo kuhusu Huduma zetu kwingineko kwenye Intaneti. Maelezo yanayokusanywa kupitia mchakato huu na mtoa huduma mwingin haituwezeshi sisi au wao kutambua jina lako, maelezo yako ya mawasiliano, au maelezo mengine ya kibinafsi ambayo yanakutambulisha moja kwa moja isipokuwa uamue kupatiana maelezo haya. Matangazo kama hayo yatawasilishwa tu inaporuhusiwa na sheria husika. Ukikosa kuruhusu kuki hizi, utakumbwa na matangazo machache zaidi yaliyobinafishwa kulingana na mahitaji yako kwenye Tovuti zetu na hautapokea matangazo yaliyobinafsishwa ya Worldcoin kwenye tovuti za wahusika wengine.

Worldcoin pia inatumia huduma ya Google. Maelezo mengi zaidi kuhusu jinsi Google inavyotumia data zako unapotumia tovuti na programu za wabia wake: https://www.google.com/policies/privacy/partners/. Wewe kutumia Huduma hizi ni dhihirisho la idhini yako kwa Worldcoin ya kuhifadhi na kufikia kuki na data nyingine kwenye kompyuta yako au kifaa chako tamba na Worldcoin kutumia huduma ya Google Analytics kuhusiana na shughuli hizo. Tafadhali soma maelezo yaliyo kwenye kiungo kilichopatianwa ili uelewe unachoidhinisha.

**10. Tunahifadhi Data Zako Kwa Muda Gani?**

Tunahifadhi data zako kwa muda ambao unahitajika ili kukupa Huduma zetu, kutimiza malengo yetu ya kibiashara, na kuambatana na majukumu yetu ya kisheria na kiudhibiti. Ukifunga akaunti yako uliyofungua nasi, tutaendelea kuhifadhi data zako kadri inavyohitajika ili kuambatana na majukumu yetu ya kisheria na kiudhibiti, pamoja na kufuatilia, kugundua, na kuzuia ulaghai, na pia majukumu ya ripoti za ushuru, uhasibu, na kifedha.

**Tafadhali kumbuka:** Blockchain ni mitandao ya wahusika wengine ambayo haina mamlaka kuu na ambayo haidhibitiwi wala kuendeshwa na Worldcoin. Kwa ajili ya hali ya teknolojia ya blockchain kuwa ya umma na isiyoweza kubadilishwa, hatuwezi kurekebisha, kufuta, wala kudhibiti ufichuaji wa data zilizohifadhiwa kwenye blockchain.

**11. Jinsi Kauli hii ya Faragha ilivyo Tofauti kwa Watoto na Vijana**

Watu chini ya umri wa miaka 18 hawaruhusiwi kutumia Huduma, na hatukusanyi data kutoka kwa watu walio na umri wa chini ya miaka 13 tukifahamu na kukiuka sheria ya Ulindaji Faragha ya Watoto Mtandaoni (Children's Online Privacy Protection Act). Ikiwa unaamini kwamba mtoto wako aliye chini ya umri wa miaka 13 amefikia Huduma bila kibali chako, unaweza kuomba data zake kufutwa kwa kuwasiliana nasi kupitia Lango letu la Maombi.

Tukijua kwamba tumekusanya data kumhusu mtoto chini ya umri wa miaka 13, tutafuta data hizo haraka iwezekanavyo. Tumechukua hatua za busara kibiashara ili kuwekea vikwazo matumizi ya Huduma kwa watu walio na umri wa angalau miaka 16. Hatutengenezi bidhaa au huduma za sokoni za kununuliwa na watoto.

**12. Jinsi ya Kuwasiliana Nasi Kuhusu Kauli hii ya Faragha**

Unaweza kuamua kufuta data zako kutoka kwenye programu ya Worldcoin. Ikiwa una maswali au wasiwasi zozote kuhusu Kauli hii ya Faragha, ungependa kutumia haki zako, au kuwasiliana na Afisa wa Faragha ya Data, tafadhali wasilisha ombi lako kupitia Lango letu la Maombi au kwa kututumia barua kwa anwani Tools For Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA. Tutajibu maombi yote tunayopokea kutoka kwa watu wanaotaka kutumia haki zao za ulindaji data kulingana na sheria husika za ulindaji data. Pia unaweza kufuta data zako kutoka kwenye ndani ya programu ya Worldcoin.

Ikiwa una wasiwasi zozote za faragha au matumizi data ambazo hazijasuluhishwa na ambazo hazikushughulikiwa mpaka ukaridhika, tafadhali wasiliana na mdhibiti ulinzi wa data katika eneo lako. Unaweza kupata mdhibiti ulinzi wa data wako hapa.